



## **MKOA WA DAR ES SALAAM**

### **UZINDUZI WA PROGRAMU YA KIATAMIZI**

### **TANGAZO LA KUFUNGUA DIRISHA LA KUPOKEA MAOMBI**

Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo (SIDO) Mkoa wa Dar es salaam linapenda kuwatangazia umma wa watanzania ya kwamba imeanza kupokea maombi ya maeneo maalum ya kulea ubunifu (kiatamizi). Watakaochaguliwa watapata fursa ya kulea ubunifu wao kwa muda wa miaka mitatu (3) na baadaye kuhitimu. Kwa kipindi chote hicho watapewa mafunzo ya kuwajengea uwezo, watahiriki semina mbalimbali, wataunganishwa na taasisi za fedha na vilevile taasisi za elimu ya juu.

#### **Sifa za muombaji:**

- Mtanzania mwenye umri wa miaka 18 na kuendelea.
- Andiko lisilozidi kurasa tatu likielezea ubunifu kwa kina na namna ubunifu huo utajengeka kuwa biashara yenye faida na tija. Weka picha kama zipo pamoja na wasifu binafsi.
- Ubunifu lazima uwe umefikia hatua ya ukomavu unaoelekea kwenye bidhaa ama huduma inayokaribia kuingia sokoni na uwe ni ubunifu wenye mtizamo wa kuleta mageuzi ya viwanda na wenye uwezekano wa kutengeneza bidhaa au huduma itakayoondoa ama kupunguza changamoto za kijamii na kiuchumi.
- Ubunifu lazima uwe wa kimageuzi na ulenge maeneo ya teknolojia, uongezaji thamani mazao ama ubunifu unaounganisha maeneo mbalimbali.

#### **Namna ya kutuma maombi:**

Tuma maombi yako kwa **Mwenyekiti wa Kamati ya Mchujo, Programu ya Kiatamizi, Shirika la Kuhudumia Viwanda Vidogo, S.L.P 22151, Dar es**

**salaam** au tuma kwenye barua pepe **[daressalaam@sido.go.tz](mailto:daressalaam@sido.go.tz)** au kupitia tovuti hii <http://www.ubunifu.or.tz> .Mwisho wa kupokea maombi ni tarehe 21/11/2019.

Watakaopita kwenye mchujo wa awamu ya kwanza watapewa taarifa kwa njia ya ujumbe mfupi au kwa kupigiwa simu ndani ya siku saba (7) baada ya kufunga dirisha la kupokea maombi.

Maombi yote lazima yaambatane na ushahidi wa malipo ya ada ya maombi isiyorejeshika ya shilingi 50,000. Waombaji watapata namba ya kumbukumbu ya kufanyia malipo kwa kutuma ujumbe mfupi kwenye namba **+255 767 270 111** kabla ya kufanya malipo.

**VIJANA NA WANAWAKE WANAHAMASISHWA KUTUMA MAOMBI.**

**NAFASI NI CHACHE.**